

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA
UBALOZI WA TANZANIA, MUSCAT, OMAN



TAARIFA MUHIMU KWA WATANZANIA WAISHIO OMAN

KUKAMILIKA KWA MFUMO WA UPOKEAJI WA MAOMBI YA PASSPORT MPYA ZA
KIELEKTRONIKI UBALAZINI

UBALOZI WA TANZANIA NCHINI OMAN UNAWATANGAZIA KUWA IDARA YA UHAMIAJI TANZANIA IMEKAMILISHA UWEKAJI MFUMO UNAOWEZESHA WATANZANIA KUOMBA PASIPOTI MPYA ZA KIELEKTRONIKI HAPA UBALAZINI. UBALOZI WA TANZANIA HAPA OMAN KUANZIA 21 JULAI 2019 UTAANZA KUPOKEA FOMU ZA MAOMBI YA PASIPOTI MPYA ZA KIELEKTRONIKI ZA WATANZANIA WALIPO HAPA OMAN KWA UTARATIBU WA KUOMBA MIADI.

CHINI YA UTARATIBU HUU, MUOMBAJI AMBAYE AMEISHAJAZA FOMU MTANDAONI, AKALIPIA DOLA 15 NA KUCHAPISHA FOMU YAKE ATATAKIWA KUOMBA MIADI KWA KUPIGA SIMU AU KUTUMA BARUA PEPE UBALAZINI ILI KUPANGIWA MIADI YA AJE LINI NA KWA MUDA GANI ILI KUKABIDHI FOMU ZAKE KWA AFISA WA PASIPOTI UBALAZINI

AFISA ATAPOKEA FOMU NA KUHAKIKI USAHIHI WA TAARIFA KWA MUJIBU WA NYARAKA ZILIZOAMBATANISHWA NA BAADA YA KURIDHIKA NA HALI YA OMBI NA VIAMBATANISHO HUSIKA ATAMPATIA ANKARA YA KULIPIA DOLA 75 ZILIZO BAKIA

BAADA YA KUPATA ANKARA MUOMBAJI ATATAKIWA KUINGIA KWENYE MTANDAO WA MALIPO YA SERIKALI <https://epay.gepg.go.tz> NA KUFUATA MAELEKEZO. MALIPO YATAKUWA TAYARI NDANI YA MASAA 24 SIKU ZA KAZI TANGU MALIPO YALIVYOFANYIKA

BAADA YA MALIPO KUKAMILIKA MUOMBAJI ATAPIGA SIMU TENA KWA AJILI YA KUPANGIWA MIADI YA KUJA KUPIGA PICHA, KUCHUKULIWA ALAMA ZA VIDOLE NA KUSAINI

NAMBA YA KUPIGA KUOMBA MIADI NI 7170 3943 NAMBA HII NI MAALUM KWA KUOMBA MIADI NA ITAKUWA WAZI KUANZIA SAA 3 (09.00AM) HADI SAA 8 (2PM JUMAPILI HADI ALHAMIS) NA ANUANI YA BARUA PEPE NI tamuscat@omantel.net.om. SIMU HIYO ITAKUWA WAZI KUANZIA TAREHE 17 JULAI 2019 KUANZA KUPOKEA MAOMBI YA MIADI.

ZINGATIA YEYOTE ATAKAEKUJA BILA MIADI HATOHUDUMIWA NA ATATAKIWA KUFUATA UTARATIBU WA KUOMBA MIADI

MNAKUMBUSHA KUWA PASIPOTI ZA SASA ZITAKOMA KUTUMIKA IFIKAPO JANUARI 2020. OMBIA PASIPOTI MPYA SASA USISUBIRI DAKIKA ZA MWISHO

IMETOLEWA NA:

UBALOZI WA TANZANIA. MUSCAT, OMAN
16 JULY 2019

